# WANGU WA MILELE

Na:Sebastian Don Ndibalema









*1.Nasema mbele ya wazazi wako (ni wewe) ni wewe niliyekuchagua (ni wewe)*
*Nasema mbele ya wazazi wangu-Ni we wangu wa moyo*
*Ninatamka mbele za Mungu (ni wewe) mtima wangu nakupatia (ni wewe)*
*Nasema mbele ya wazazi wangu-Ni we wo mtima gwange*
*2.Unawaacha wazazi wako (ni wewe) mwili mmoja tunakuwa (ni wewe)*
*Nami nitakupenda milele-Ni we wangu wa moyo*
*Ninawaacha wazazi wangu (ni wewe) mwili mmoja tunakuwa (ni wewe)*
*Nami nitakupenda milele-Ni we wo mtima gwange*
*3.Ndi-we mama wa watoto wangu (ni wewe) Mwenyezi Mungu kanipatia (ni wewe)*
*Karibu kwetu kipenzi changu-Ni we wangu wa moyo*
*Ndi-we baba wa watoto wangu (ni wewe) Mwenyezi Mungu kanipatia (ni wewe)*
*Nakuja kwenu kipenzi changu-Ni we wo mtima gwange*
*4.Nawashukuru wazazi wako (ni wewe) ua zuri wamenilelea (ni wewe)*
*Namshukuru Mwenyezi Mungu-Ni we wangu wa moyo*
*Nawashukuru wazazi wako (ni wewe) lulu yangu walinitunzia (ni wewe)*
*Haki ya Mungu ninakupenda-Ni we wo mtima gwange*